*Sanduku la Injili la Watoto*

# RASILIMALI ZA MAFUNZO









Sanduku la Injili la Watoto

# RASILIMALI ZA MAFUNZO

Agosti 2018

CHILDREN'S gospel box

Rasilimali za Mafunzo za The Children's Gospel Box © 2018
Imechapishwa na Foursquare Missions Press for The Children's Gospel Box
Pamoja na Mizizi Mobile Missions Press © 2020
Imetafsiriwa na Tegemea Mbise
Imehaririwa na Stacy Collins

Jifunze zaidi kuhusu The Children's Gospel Box huko cgbox.org.

**Wasiliana nasi:**

1-888-635-4234 ext. 4420

gospelbox@foursquare.org

Utafute...

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 5 |
| Orodha ya Yaliyomo Kwenye Children's Gospel Box | 7 |
| Viwango vya Kukumbuka | 9 |
| Trakti za Injili | 10 |
| Kuongoza Mtoto kwa Kristo | 12 |
| Filamu ya YESU kwa Watoto | 16 |
| Hadithi ya Msalaba | 18 |
| Michezo ya Marudio ya Biblia | 20 |
| Michezo ya Kukariri Mistari ya Biblia | 22 |
| Mawazo ya Kufundisha Biblia kwa Ubunifu | 24 |
| Kuishi Maisha ya Kikristo – Majibu | 26 |
| Kutumia Vikaragosi Katika Kufundisha Watoto | 29 |
| Kitabu cha Injili Isiyo na Maneno na Bangili | 33 |
| Vijiti vya Sifa | 35 |
| Tic Tac Toe (Mchezo) | 36 |
| Karatasi ya Mpango wa Somo | 39 |

## UTANGULIZI

# Kupeleka NENO kwa Watoto wa DUNIA!

***NANI:*** Foursquare Missions Press, pamoja na uongozi wa Dr. Mary Lou Canata, walianzisha The Children's Gospel Box (CGBox) mnamo 2002. Wakurugenzi na wanachama wa sasa wanaongoza timu ya kujitolea ambao wanashirikiana na kanisa la Amerika na makanisa ya kimataifa kupata rasilimali na kutoa mafunzo kwa viongozi wa huduma ya watoto ulimwenguni kote.

***NINI:*** The Children's Gospel Box (CG Box) ni "sanduku" lililojazwa na rasilimali za uinjilishaji wa watoto na za uanafunzi. Kila "sanduku" lina vifaa vya kutosha kufikia watoto 150. Vile vile muhimu kama rasilimali ni mafunzo ambayo inaambatana na kila CG Box lililotumwa. Zaidi ya viongozi wa huduma za watoto 15,000 ulimwenguni kote wamefunzwa na wamepewa rasilimali kupitia huduma ya CG Box.

***VIPI:*** Huduma ya CG Box inategemezwa na michango. Kwa kukusanya chenji katika sanduku la chenji, watoto Amerikani wametoa masanduku maelfu kwa mataifa 55. Pia, makanisa yanafadhili masanduku, na timu ndogo za utume zinayanunua.

***WAPI:*** Mataifa 55 ambayo yameyapokea CG Boxes ni Asia, Asia Ndogo, Afrika, Mataifa ya Kiarabu, Amerika ya Kilatini, Karibiani, Amerika ya Kusini, na Ulaya.

***GHARAMA:*** Tunakadiria kuwa kila CG Box linagharimu dola za kimarekani $150 kwa vifaa vyote na gharama za usafirishaji. Kazi nyingi hufanywa na wajitoleaji, ambayo imeruhusu kuweka gharama ya chini.

***KWA NINI:*** George Barna, mtu mashuhuri kwenye taaluma ya takwimu alisema, “Huduma ya watoto ni moja wapo ya uwanja wa misheni wa kanisa leo.” Na hitaji la rasilimali za huduma za watoto ni kubwa. Ufanisi wa rasilimali na mafunzo umeonyesha kuwa The Children’s Gospel Box ndio jibu la hitaji hili.

# Orodha ya Yaliyomo Kwenye Children's Gospel Box

Kabla ya kuanza kutumia yaliyomo kwenye sanduku hili, tafadhali soma utangulizi huu. Tunaamini kwamba kupitia utumiaji sahihi wa Sanduku hili la Injili, Neno la Mungu litapandwa ndani ya mioyo na akili za watoto ambao hawakuwahi kusikia Habari Njema.

## 1. Fasihi

The Children's Gospel Box (CG Box) limejaa fasihi zitakazotumiwa kufikia watoto. Baadhi ya haya ni: trakti *"Ahadi Kubwa Zaidi"* kulingana na filamu ya YESU kwa Watoto, trakti *"Heri ya Siku ya Kuzaliwa"* ambayo inasherehekea siku za kuzaliwa asilia na za kiroho, trakti ya wokovu inayoitwa *"Tia Linda"* kutumiwa katika ujamii au mijini, na kitabu cha kazi *"Kuishi Maisha ya Kikristo,"* ambacho ni kozi ya kufuata majuma sita kwa watoto walio na miaka 8 hadi 12.

## 2. Misaada ya Biblia kwa Njia ya Kuona

Watoto hukumbuka 90% ya wanayoona na kusikia na kusema na kufanya. Kwa hivyo kufundisha Biblia kwa ubunifu ni muhimu. Baada ya yote, tunatumikia Mungu aliye mbuni sana! Baadhi ya misaada hiyo ya kuona ni: "EvangeCube" iliyotumiwa kushirikisha ujumbe wa Injili, "flannel graph" (picha juu ya vitambaa maalum) iliyotumiwa kufundisha masomo ya Biblia, na "Habari ya Msalaba," ambayo inatumia karatasi ya kawaida.

## 3. Vikaragosi

Vikaragosi vimetolewa vitumiwe katika jamii kuwaalika watoto kuhudhuria mikutano kanisani, wakati wa kufikia watoto waliopotea ili kuvutia umakini wa watoto, na mara kwa mara kusaidia kufundisha masomo ya Biblia. Hakikisha unafanya mazoezi na kikaragosi mapema, kabla ya mkutano. Na ikiwa vikaragosi zaidi vinahitajika, watu wazima na watoto wanaweza kutengeneza kikaragosi chao wenyewe.

## 4. Rasilimali za Injili Zisizo na Maneno

Vifaa hivi vinatoa njia rahisi, njia ambayo inaweza kuendelea kuzaa matunda tena kwa viongozi, watu wazima, na watoto kushiriki Injili. Watoto wanapojifunza wenyewe, wataweza kurudia hadithi na kushiriki Habari Njema na wenzao. CG Boxes yanaweza kuwa na vitabu vya vitambaa maalum au vitabu vilivyochapishwa, bangili au mnyororo wa funguo na vingine zaidi!

## 5. Vijiti vya Sifa

Vijiti vyenye riboni ni “Kijiti cha Sifa,” ambavyo watoto wanafurahia sana. Hivi hutumiwa katika ibada kuwatia moyo watoto kumsifu Bwana.

## 6. Tic Tac Toe (Mchezo)

Vitambaa maalumu pamoja na vipande vidogo vidogo ndiyo Tic Tac Toe. Mchezo huu hutumiwa kucheza michezo ya marudio darasani.


Vifaa vingine vinavoweza kujumuishwa kwenye CG Box ni: *Filamu ya YESU kwa Watoto*, kitambaa cha hadithi za Biblia, na kadhalika.

# *Wanafunzi wanakumbuka hadi...*


**10%** ya wanayo**SIKIA**




**30%** ya wanayo**ONA**



**50%** ya wanayo**ONA**
na ku**SIKIA**




**70%** ya wanayo**ONA**
na ku**SIKIA**na ku**SEMA**



**90%** ya wanayo**ONA**
na ku**SIKIA**
na ku**SEMA**
na ku**FANYA!**




# Trakti au Vipeperushi vya Injili

## Kwa Nini Vipeperushi vya Injili?

Imesemekana kuwa hakuna chochote chenye gharima ndogo, huenda mbali zaidi, hubaki muda mrefu zaidi, au inasema bora kuliko trakti au vipeperushi vya Injili.





- Trakti zinaweza kuwa kifaa cha uinjilisti kumwongoza mtoto kwa Kristo.
- Trakti zinaweza kuwa vifaa vya kumfuatilia mtoto na uthibitisho kuwa mtoto amefanya uamuzi kwa ajili ya Kristo.
- Trakti zinaweza kuwa kifaa cha uanafunzi kufundisha watoto jinsi ya kuwaongoza wengine kwa Kristo.
- Trakti zinaweza kuwa mwongozo wa mafunzo kwa viongozi wa huduma za watoto.
- Trakti zinaweza kuwa kifaa cha kufundisha mtu mwenye upungufu wa misamiati au uwezo mdogo wa kusoma.
- Trakti zinaweza kwenda nyumbani pamoja na watoto na zinaweza kusomwa na wazazi wao.

## Jinsi ya Kutumia Trakti za Injili




- Kwanza, ujue ni nini trakti inazungumzia.
- Muhimu zaidi, SALA! Mtu hawezi kumshawishi mtu yeyote kumpokea Kristo; wala trakti haiwezi; Roho Mtakatifu tu ndiye anayeweza kufanya hivyo. Omba kwamba Roho Mtakatifu azungumze na moyo wa mpokeaji ili apate kuelewa ujumbe huo na kumpokea Kristo.
- Wasiliana na macho na tabasamu. Tabasamu za kweli wakati mwingine ni ngumu kuona, lakini zinaweza kuunda ufunguzi wa kutumia trakti.
- Tunza trakti katika hali nzuri. Hakikisha ziko safi na zenye ubora, badala ya kuonekana kama zimekuwa mfukoni kwa siku kadhaa.

## *Kijitabu cha Ahadi Kubwa Zaidi*




Kawaida trakti hii inapaswa kutumiwa pamoja na Filamu ya YESU kwa Watoto. Baada ya filamu kuonyeshwa, gawanya watoto wa miaka 5 na chini kutoka kwenye watoto wakubwa. Watoto hawa wachanga wanahitaji kuhudumiwa kwa kiwango kinachofaa kwa umri wao.

Watoto wenye umri wa miaka 6 na zaidi wanapaswa kuhamishwa katika vikundi vya watu 10 au chini. Mtu mzima atapitia trakti hiyo na watoto na atawapa watoto nafasi ya kumkubali Yesu kama Mwokozi wao.

Kila mtoto atapeleka nakala yake ya trakti hiyo nyumbani.
(Tazama ukurasa uliojumuishwa wa “Filamu ya YESU ya Watoto” kwa habari zaidi.)

### Yesu anataka watoto waje Kwake!

*Watoto walipoletwa kwa Yesu ili aweze kuweka mikono yake juu yao na kusali, wanafunzi walijaribu kuwazuia. Yesu aliitikia, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao" Mathayo 19:13-14.*

## Miongozo 10 Ya Kumwongoza Mtoto Kwa Imani Katika Kristo

### 1. MUNGU ANAKUPENDA

- Mfanye mtoto ajue kuwa Mungu ndiye aliyemwumba. Anajua kila kitu juu yetu (Warumi 5:8). Na kwamba yeye ni muhimu kwa Mungu kwa sababu Mungu anamtakia vitu vizuri.
- Hakuna kitu kitakachomfanya Mungu aache kutupenda, hata mambo mabaya ambayo tunafanya au mambo mazuri ambayo hatufanyi (1 Yohana 4:16 na Warumi 8:38-39).

### 2. SISI SOTE NI WENYE DHAMBI

- Dhambi ni kufanya vitu ambavyo Mungu hataki tufanye nakutofanya kile ambacho Mungu anataka tufanye.
- Msaidie mtoto kuelewa kuwa yeye ni mwenye dhambi. Sisi sote tumetenda dhambi (Warumi 3:23).
- Adhabu ya dhambi ni kifo. Kwa hivyo, Yesu Kristo, ambaye ni Mwana wa Mungu, alichukua adhabu kwa ajili yetu alipokufa msalabani na akafufuka (Warumi 6:23).
- Yesu alikufa msalabani na akafufuka ili kulipia dhambi zetu. Yesu anaishi leo!

### 3. TUNAWEZA KUWA SEHEMU YA FAMILIA YA MUNGU

- Kwa sababu ya kile Yesu ametufanyia, tunaweza kujiunga katika familia ya Mungu.
- Tumia Yohana 1:12 (ambayo ilifafanuliwa) kumsaidia mtoto kuelewa kuwa tunaamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, Mwokozi wetu, na Mungu hutupa nguvu ya kuwa wana na binti zake.

## 4. KAZI YAKO NI KUMWAMINI NA KUMKARIBISHA

- Msaidie mtoto kuelewa kuwa anahitaji kumwambia Mungu anamwamini Yesu, kukiri kwamba yeye amefanya makosa, kumwomba Mungu amsamehe, na kumkaribisha Yesu kuwa Mwokozi wake na kuwa msimamizi wa maisha yake. Hivi ndivyo tunapokea zawadi kuu ya Mungu ya wokovu (Waefeso 2:8).

## 5. ZUNGUMZA NA MUNGU

- Mhimize mtoto kuzungumza na Mungu kwa kutumia maneno yake mwenyewe. Ikiwa mtoto hana maneno msaidie kuyapata, msaidie kuomba sala rahisi, ukirudia kifungu kwa kifungu. Mkumbushe mtoto afikirie kwa uangalifu juu ya maneno anayoyarudia, na ayaseme kama ni yake mwenyewe.

> *Mungu mpendwa, Muumba wangu,*
> *Asante kwa kunipenda. Ninaamini moyoni mwangu kuwa Yesu Kristo ni Mwana wako. Ninaamini alichukua adhabu ya dhambi zangu wakati alipokufa msalabani na akafufuka tena. Najua nimetenda dhambi na nimefanya mambo mabaya. Sijatii. Tafadhali unisamehe na uondoe hatia na aibu yangu. Nipe nguvu ya kusema "NDIYO" kwako na "HAPANA" kwa vitu vibaya. Bwana Yesu, tafadhali njoo maishani mwangu kama Mwokozi wangu na Mfalme. Nataka kukutii. Nisaidie kukufuata, na jifunze kuishi kwako. Nifanye niwe sehemu ya Familia Yako. Wewe ni Mungu wangu, na mimi nakuabudu.*

## 6. MAISHA YA KIKRISTO

- Fafanua kwa mtoto kwamba kumwalika Kristo kuwa Mfalme na Mwokozi wake haimaanishi kuwa atakuwa kamili tangu wakati huo na kuendelea. Mtu hasipotii au akifanya kitu kibaya, mtu huyo anatakiwa kumwambia Mungu kile alichofanya, haraka iwezekanavyo. Fafanua kuwa Mungu anaahidi katika Neno Lake kwamba tunapokubali kwamba tumefanya mabaya na kumwambia, atatusamehe na kutusafisha na dhambi zote (1 Yohana 1:9).

- Msaidie mtoto kuamua kumjua Yesu vizuri kila siku. Mungu ndiye atakayewapa nguvu na uwezo wa kuwa kama Yesu. Kuwa kama Yesu inamaanisha kuwa na tabia kama Yake ya upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, wema, uaminifu, upole na kujitawala, ambazo ni Matunda ya Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:22-23).
- Kumjua Yesu vizuri, tunapaswa:
    - Kuongea na Mungu na kusikiliza sauti yake.
    - Kumwabudu na kumsifu Mungu. Mwambie "Asante."
    - Kusoma, kujifunza na kukariri Biblia, kuanzia na Agano Jipya.
    - Kwenda kanisani ili ujifunze zaidi kuhusu Mungu.
    - Kuongea na wengine kuhusu Yesu na uwasaidie kumjua Yeye.
    - Kufanya mazoezi ya utii kwa kusema “Ndiyo” kwa Mungu na “Hapana” kwa dhambi.

## 7. KUNA ADUI

- Mfundishe mtoto kwamba ingawa shetani ni mwongo ambaye atajaribu kumwambia kwamba hakuna mabadiliko yaliyotokea baada ya Yesu kuwa Mwokozi wao, Mungu ana nguvu zaidi kuliko shetani.
- Msaidie mtoto kuelewa kwamba shetani anaweza kujaribu kumfanya ahisi kuwa hajasamehewa na kwamba bado anapaswa kuhisi ana hatia. Lakini Biblia inasema kwamba wakati Mungu anasamehe dhambi zetu, huzitupa katikati ya bahari (Mika 7:19) na hatazikumbuka tena (Waebrania 10:17).

## 8. SHIRIKISHA

- Mwelekeze mtoto amwambie mtu mwingine kuwa anaamini katika Yesu kama Mwokozi na anataka kumtumikia maisha yake yote (Warumi 10:9-10).
- Msaidie mtoto kuelewa ni Amri Kuu au Utume Mkubwa kuwaambia wengine Habari Njema.


## 9. OMBA

- Ombea mahitaji maalum ya mtoto, umwombe Mungu amsaidie mtoto kumjua na kujifunza zaidi juu yake kila siku ya maisha yake.
- Endelea kumwombea mtoto baada ya kipindi hichi. Andika maelezo yenye jina lake na tarehe ili kutumika kama ukumbusho wa maombi.

## 10. UFUATILIAJI

- Jitolee kuwa na darasa au masomo ya Biblia na mtoto kwa kumfuatilia ili aweze kujifunza kutembea na Yesu na kukua katika uhusiano naye.

# "Filamu ya YESU" Kwa Watoto




Filamu hii inasimulia hadithi ya Yesu, kama inavyoonekana kupitia macho ya watoto. Inafuata maisha ya Benjamini, Kalebu, Sara, Yoeli, Lea na Nathani, walioishi huko Yerusalemu karibu miaka 30 A.D.

Inaonyesha hadithi za Mtu kutoka Nazareti ambaye anaponya wagonjwa na kufufua wafu. Wakati wanajitahidi kuelewa yote, wanamtazama Yesu kutoka kwenye umati, na kumfuata ili kuona mtu huyu mzuri, ambaye anapenda watoto, atafanya nini baadaye. Wanamwona akisalitiwa, akishtumiwa vibaya, akisulubiwa na akazikwa. Lakini, wanakumbuka ahadi ya Yesu na wanaamini watamwona tena. Watoto wa kila umri watafurahia hadithi hii inayovutia inayoeleza maisha ya kweli ya Yesu kutoka kwa mtazamo wa mtoto.

Toleo hili lililohaririwa kwa madhumuni kwa ajili ya kuacha sehemu ngumu kutoka kwenye kusulubiwa kwa Kristo na kuifanya iwe sawa kwa watoto.

## Jinsi ya Kutumia DVD Kwa Ufanisi

DVD hii ina urefu wa dakika sitini na mbili (62). Hapa kuna maoni kadhaa kwa ajili ya matumizi yake:

Panga mkutano au kusanyiko la masaa mawili. Onyesha sehemu ya kwanza ya sinema (unapumzika wakati wa saa 37:52). Tenganisha watoto kwa vikundi vidogo na uwajulishe kile ambacho wanakaribia kukiona katika mateso ya Yesu, kusulubiwa, na ufufuo. Basi ruhusu watoto kutazama sehemu iliyobakia ya sinema. Baadaye, warudishe kwenye vikundi vidogo kwa majadiliano kwa kutumia trakti (hapo chini).

Karibisha mkutano wa kusanyiko la siku 2. Onyesha sehemu ya kwanza katika mpangilio mmoja na sehemu ya pili siku inayofuata, na kuvifuatlia vikundi baadaye.

## *Kijitabu cha "Ahadi Kubwa Zaidi"*




Hakiki DVD na timu yako na wale ambao watakuwa wakihudumia watoto mwisho wa onyesho. Trakti itapewa kila mtoto kwenye kikundi kidogo cha watoto kumi. Watoto wanapaswa kufuatisha kama mwalimu wao wanavyosoma, au wanaweza kusoma kwa pamoja. Kwa kushirikiana na kupanga, hii inaweza kuwa wakati wenye maana sana katika maisha ya mtoto.

Baada ya kuona filamu na kusoma trakti, sasa ni wakati wa wale wanaotamani kumpokea Yesu kama Mwokozi wao kufanya hivyo. Kiongozi ataongoza na atawaambia watoto warudie anachosema kiongozi. Mpe mtoto uthibitisho wa kibiblia kuwa yeye sasa ni sehemu ya familia ya Mungu. (Tazama ukurasa uliojumuishwa kuhusu jinsi ya kumwongoza mtoto kwa Kristo kwa habari zaidi.)

Kumbuka: Ikiwa kikundi chako kinahudhuriwa na watoto ambao hawajaanza shule / watoto wa chekechea, inashauriwa kwamba mipango ipangiliwe mapema kwa undani kwa walimu waliopagwa kuchukua watoto hawa katika vikundi vyao, na kuongea nao kwa kutumia picha za trakti, nk.

# Hadithi ya Msalaba

## Kuandaa

Fanya mazoezi sana kwa kutumia kipande cha karatasi cha inchi 8.5 x 11. Soma hadithi hiyo mpaka iwe na mtiririko mzuri, kunja na rarua karatasi kama hadithi ilivyosema.

"Hadithi ya Msalaba" imetolewa na huduma ya Child Evangelism.

## Hii ndio hadithi:

*Kulikuwa na mtu ambaye alipenda kuwaambia watu kuhusu Yesu. Katika nchi yake, hata hivyo, watu hawakuruhusiwa kuzungumza kuhusu Yesu. Hii hufanyika mahali mbali mbali ulimwenguni hata leo, lakini watu wanaendelea kuwaambia wengine kuhusu Habari Njema ya Yesu. Na hiyo ndivyo mtu huyu alifanya pia. Hakuacha tu. Kwa hivyo siku moja, aliwekwa gerezani kwa kufanya hivi.*

*Huko gerezani, alianza kuongea na walinzi na wafungwa wengine kuhusu Yesu. Alionywa na afisa mkuu kwamba atauawa ikiwa asingeacha kuongea kuhusu Yesu. Lakini, afisa huyo alisema ikiwa mtu huyo angemwonyesha jinsi msalaba unaonekana, hatakufa.*

*Afisa huyo alimpa mtu kipande cha karatasi na kumwambia, "Ikiwa unaweza kutengeneza msalaba kwenye karatasi hii kwa kukatwa moja tu kutoka kwa upanga wangu, basi nitamwamini Mungu wako."*

*Usiku huo, mfungwa alisali na kusali, akimwomba Bwana amwonyeshe cha kufanya. Mtu huyo alianza kukunja kona moja ya karatasi chini kama hivi kisha akafunika kona nyingine chini (uwaonyeshe watoto). Kisha akaikunja nusu mara nyingine zaidi kwa namna ile ile (onyesha watazamaji).*

*Mtu huyo alilala. Asubuhi, afisa huyo akaja na upanga. Alisema, "Amka. Nionyeshe msalaba." Mtu huyo alishika kipande cha karatasi kilichokunjwa. Na afisa huyo akata kipande cha karatasi kama hivi (kata kipande cha karatasi katikati). Na alipokuwa akichukua vipande vipande na kuvikunjua, mtu huyo alipata MSALABA hii (onyesha msalaba)!*

*Unapofika hapo, soma kutoka kwa Biblia hadithi ya kusulubiwa na utumie msalaba kuzungumza kuhusu "kwa nini" Yesu alilazimika kufa.*


**UKIPENDA** tumia vipande vilivyobaki kuandika maneno haya kwa Kiingereza:

**HELL / JEHANAMU** Jinsi msalaba ulivyotuokoa kwenye adhabu


**LOVE / UPENDO** Jinsi msalaba ulivyokuwa mfano bora wa upendo katika historia yote

**LIFE / MAISHA** Jinsi Yesu alivyofufuka tena baada ya msalaba ili tuweze kuwa na uhusiano naye!


## Maelezo ya Kuona





**HELL / JEHANAMU**



**LOVE / UPENDO**



**LIFE / MAISHA**



## Michezo ya Marudio ya Biblia

Watoto watatilia maanani zaidi wakijua mchezo wa marudio ya Biblia unakuja mwisho wa somo. Michezo hii inaweza kuchezwa kwa mtu mmoja mmoja au kwa timu.

**Vitu vya Kukumbuka:**

1. Kuwa mwenye haki
2. Kuwa mbunifu
3. Usicheze mchezo huo huo kila wiki
4. Dumisha nidhamu
5. Kuwa mwenye shauku
6. Cheza pamoja na watoto
7. Pitia hadithi unapouliza kila swali
8. Kuwa na matarajio ya hali ya juu, lakini siyo yasiyowezekana
9. Toa tuzo mshindi wa kwanza na wa pili
10. Acha kucheza wanapofurahiya sana. Waache wakitaka kucheza zaidi, badala ya kucheza hadi wawe na kuchoka.

### *Mchezo # 1:* Box Toss (Tupa Sanduku)

Pamba sanduku. Kata kishimo kwenye kifuniko cha sanduku inchi 6 kwa inchi 4. Baada ya mtoto kujibu swali kwa usahihi, anaruhusiwa kutupa mifuko ya maharage au vitu vingine kutoka umbali wa futi 4 hadi 5 kwenye sehemu yenye uwazi ya sanduku. Moja ikiingia shimoni, mtu binafsi au timu inapokea alama moja.

### *Mchezo # 2:* Bible Relay (Mashindano ya Mbio ya Biblia)


Gawanya darasa katika timu mbili. Kila timu ipange mstari, mtu mmoja mbele na mwingine nyuma. Pata viongozi wawili (watu wazima) na uwape kila mmoja nakala ya maswali ya marudio. Mtoto wa kwanza katika kila mstari anaulizwa swali la marudio na kiongozi. Ikiwa anajibu kwa usahihi, mtoto huyo huenda mwisho wa mstari. Ikiwa jibu sio sahihi, mtu huyo hukaa, anabaki pale pale. Timu ya kwanza kuwa na mtu wao aliyeanza kuzunguka nyuma kwenda mbele ya mstari wanashinda.

## Mchezo # 3: Zonk

Kata vipande 10 au 15 vya karatasi nzito, inchi 2 x 5 kila kimoja. Juu ya kila moja iandikwe idadi ya alama (100, 500, 1000). Fanya nyingine iwe "Chukua mbili" au "Jaribu tena" na machache neno "ZONK." Mtoto anapojibu swali la marudio, huchukua kadi na kufuata maagizo au kupata alama kama ilivyoelekezwa. Ikiwa amechukua moja ya kadi za ZONK, timu inapoteza alama zote zilizokusanywa.

## Mchezo # 4: Go Fish (Vua Samaki)

Tumia muundo hapo chini, tengeneza "samaki" 10 au 15 na uambatishe “paper clip” karibu na kinywa cha kila mmoja. Andika nambari kadhaa nyuma ya kila samaki (100, 250, 500, 1000). Tengeneza ndoano ya uvuvi kwa fimbo, kamba na sumaku kwenye mwisho wa kamba. Mtoto anapojibu swali la marudio, anaweza "kwenda kuvua samaki" kwa ajili ya timu yake na kupokea idadi ya alama kwa samaki alioshika.



# Michezo ya Kukariri Mistari ya Biblia

Kusudi ni kuwafanya watoto wakariri Neno la Mungu. Hii ni bora kufanywa na kurudia. Kurudia mistari kwa pamoja pamoja angalau mara 3 kabla ya kuanza mchezo huu.

## Mchezo # 1: Shinda Saa

Andika mstari kwenye karatasi na ukate katikati ya kila neno. Changanya maneno kwenye mstari ya kumbukumbu. Halafu watoto waanze kuweka maneno kwenye mpangilio sahihi. Mtoto anayefanya hivyo kwa haraka anakuwa ameshinda. Baada ya kila awamu, watake wanafunzi warudie mstari.

## Mchezo # 2: Nini Kinakosekana?

Andika mstari kwenye karatasi na ukate katikati ya kila neno. Weka mstari mbele ya darasa. Acha watoto wote wafungue macho yao. Ondoa neno moja. Mtoto ambaye kwanza anaweza kujua ni neno lipi linakosekana anashinda! Mtoto huyo lazima asome mstari yote. Kisha endelea kucheza hadi maneno yote yatakapokwisha.

## Mchezo # 3: Piga Makofi

Weka mstari mbele ya darasa. Mtoto mmoja ageuke nyuma, ageuzie mgongo ule mstari. Mwalimu au mtoto mwingine aonyeshe neno moja. Watoto wengine wote wanaona ni neno gani lililochaguliwa. Mtoto aliyechaguliwa kugeuzia mgongo wake ubaoni aendelee kukaa vile vile, watoto wengine watasema mstari kwa sauti. Wanapokuja kwenye neno lililochaguliwa, wanapiga makofi kwa pamoja badala ya kutaja neno hilo. Mtoto atakuwa ameshinda akisema ni neno gani limechaguliwa.

## Mchezo # 4: Joto na Baridi

Kitu kidogo kinahitajika. Mtoto mmoja anatoka nje ya chumba. Mtoto mwingine anaficha hicho kitu. Kikundi kinaendelea kurudia mstari mara kwa mara kama mtoto anapoingia ndani akitafuta kile kitu. Yule mtoto anapokuwa mbali na kile kitu, kikundi kinarudia mstari polepole, na mtoto anapokaribia kitu hicho, darasa linasema mstari hiyo kwa sauti wa juu zaidi. Akikaribia kile kitu, darasa linasema mstari hiyo, bila kuacha. Mtoto anapozidi kuwa mbali na kitu, darasa inasema mstari kwa sauti ndogo zaidi. (Huu ni mchezo mzuri kutumiwa wakati wa kufundisha mstari mrefu, kwa hivyo watoto wanaweza kuendelea kusema mstari mzima.)

## Mchezo # 5: Uso kwa Uso

Watoto wawili wanaangaliana. Mmoja anasema neno la kwanza katika mstari, kisha mtoto mwingine anasema neno la pili. Kisha inarudi kwa mtoto wa kwanza kusema neno la tatu. Hii inaendelea hadi mtoto mmoja asiweze kutaja neno linalofuata au kushidwa kusema neno kwa usahihi. Mshindi anampa mtu mwingine changamoto ya kujaribu kumshinda.

## Mchezo # 6: Changamoto ya Bahasha

Andika mstari kwenye karatasi mbili tofauti. Kata kila mstari kwa namna moja. Weka kila mstari kwenye bahasha tofauti. Mwalimu atakapowaambia waanze, watajaribu kuziunganisha zile mstari kwa usahihi kwa kuweka maneno kwenye sakafu au kwenye meza. Wa kwanza kumaliza atakuwa mshindi.

## Mchezo # 7: Kiazi Moto

Waagize watoto kusimama kwenye duara na kupitisha kitu (kama kiazi). Wakati kitu hicho kinapokuja kwa mtoto, anasema neno la mstari inayofuata. Mwisho wa mstari, mtu yeyote aliye na kitu hicho yuko anatoka nje ya duara. Mchezo unaendelea, ukirudia mstari tena na tena hadi mtu mmoja tu anasalia kama mshindi.



# Mawazo ya Kufundisha Biblia kwa Ubunifu

Imethibitishwa kuwa watu huhifadhi zaidi yale wanayoona, wanayosikia, wanayosema na wanayofanya. Kwa hivyo hatutaki kufundisha kwa njia ambayo inaruhusu watoto kuSIKIA tu - lakini kupata uzoefu zaidi. Hadithi za Biblia zinaweza kuwa hai ikiwa zinawasilishwa kwa njia za ubunifu!

**Hapa kuna maoni kadhaa ya njia za kufundisha Biblia kwa ubunifu, pamoja na misaada ya kuona iliyotolewa:**

## *Wazo # 1:* Sanaa, Sanaa na Sanaa Zaidi

Kutumia picha, chora hadithi kama inavyosimuliwa. Mwalimu au msaidizi anaweza kuchora mchoro. Sio lazima kuwa kito cha kushangaza. Watoto watafurahi tu KUONA kitu wanaposikiliza hadithi.

## *Wazo # 2:* Mtunga Hadithi

Tumia kofia au viwasilishi vingine, mwalimu au msaidizi anaigiza hadithi hiyo, akibadilisha kofia au kanzu kulingana na ni nani anayeongea. Kwa mfano, katika hadithi ya Adamu na Hawa, wakati hadithi inamtaja Adamu, vaa kofia ya mwanaume. Wakati hadithi inamtaja Hawa, badilisha kuwa kofia ya mwanamke au kanzu. Wakati inamtaja adui, vaa kofia ya kijani au kofia ya ngozi ya nyoka. Inaweka umakini kwa watoto kwa sababu mtu mmoja anacheza kila sehemu ya hadithi. Kwa namna nyingine, tumia mtoto na umruhusu awe muigizaji pekee.

## *Wazo # 3:* Hadithi Inayosafiri

Gawanya Hadithi ya Biblia katika sehemu 5. Anza mbele ya kikundi chako na ufundishe hatua ya kwanza. Kisha zunguka kwa upande wa kulia wa kikundi na ufundishe hatua ya pili. Ifuatayo, nenda nyuma ya kikundi kufundisha hatua ya tatu (ndiyo, watoto wote watageuka kutazama!). Baada ya hayo, nenda upande wa kushoto wa kikundi chako kufundisha hatua ya nne. Na mwishowe, rudi mbele ya kikundi kufundisha hatua ya mwisho na matumizi.

## Wazo # 4: Viwasilishi Kwenye Begi

Chagua sehemu 3 au 4 za hadithi ili kusisitiza. Halafu, fanya kazi ya kupata kiwasilishi cha kuwakilisha kila sehemu hizi za hadithi. Kwa mfano, katika hadithi ya tanuru ya moto, kukusanya sanamu (kama ile watoto wa Waebrania waliinama chini), chombo cha muziki (kwa muziki uliowasukuma wainame), na kitu kama moto (kitambaa chekundu, mwanga, au picha ya moto). Ikiwezekana, weka viwasilishi hivyo kwenye begi. Halafu, hadithi inaposimuliwa, toa kiwasilishi kinachoendana na uwaulize watoto kina maana gani. Kisha fafanua jinsi kitu hicho kinasimulia hadithi.

# Kuishi Maisha ya Kikristo - Karatasi ya Majibu

Kitabu hiki ni kozi ya wiki sita ya kuwafuatilia watoto wenye miaka kati ya 8 na 12 baada ya kumkiri Yesu Kristo kama Mwokozi. Tunashauri wakati na mahali maalumu palipoandaliwa kwa ajili ya hawa waumini wapya. Mwalimu atakamilisha nakala yake na kufundisha somo moja kila wiki wakati wa darasa. Utambuzi wa kukamilika unaweza kupangwa mwishoni mwa wiki ya sita kwa kuwasilisha darasa kanisani/kwenye idara ya watoto au kwa kutoa tuzo.

## Somo la 1

1. Majibu yanaweza kutofautiana
2. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote " 1 Yohana 1:9
3. Usitii - Usishirikiane - kwa baadhi tu ya watu - chukia
4. Ndiyo - Ndiyo - Hapana - Ndiyo - Ndiyo
5. Jina la mtoto - jina la mtoto - jina la mtoto
6. Kutotii - Makosa - Ubaya
7. Ndiyo
8. Mwana wa Mungu
9. Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama Maandiko yalivyosema
10. Tukiziungama - atuondolee
11. ninyi - mna - Mwana
12. Kristo

## Somo la 2

1. Kuwa mwaminifu wakati wote - Onyesha fadhili kwa kila mtu - Mheshimu Mungu katika vitu vyote - Watii wazazi - Wapende wengine
2. Atatusamehe dhambi zetu
3. Ndiyo - ndiyo - ndiyo
4. X - Ninapaswa kuzungumza na Mungu katika sala kila siku
5. Shetani
6. Kweli - Kweli - Si Kweli
7. Mungu

8. X - Hapana
9. Kariri mstari
10. "Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."
    Mathayo 28:20b

## Somo la 3

1. soma Biblia
2. Mjue Mungu - Jifunze kuhusu Yesu
3. X - Ninapaswa kusoma Biblia yangu kila siku
   X - Biblia ni Neno la Mungu
4. Mungu - Mwalimu wa Shule ya Jumapili - Mchungaji
5. taa – mwanga
6. "Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe." Mathayo 24:35
   "Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi." Zaburi 119:11
   "Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu." Zaburi 119:105
7. Idadi ya Biblia nyumbani kwa mtoto
8. Mtoto anamwandikia Mungu jinsi ambavyo Biblia ina maana kwake
9. Mstari wa Biblia ambayo mtoto anaipenda zaidi

## Somo la 4

1. X - Kusali / kuomba
2. Macho yake huwaelekea wenye haki
   Masikio yake husikiliza maombi yao
3. Kila wakati / Kila mara
4. Mahali popote
5. K – Naweza kuongea na Mungu wakati wowote, mahali popote
   K – Kuungama ni kukiri kwa Mungu kosa langu
   K – Ninapaswa kuombea wengine
   K – Kuomba kila siku ni tabia nzuri
6. Kariri
7. Hapana – Ndiyo – Ndiyo

## Somo la 5

1. Mahali pa kumwabudu Mungu
   Mahali pa kuimba na kusifu
   Mahali pa kujifunza zaidi kuhusu Mungu
2. tusiache - pamoja
3. Hapana – Ndiyo – Ndiyo
4. Kanisa
5. Kuabudu - Kuimba - Kutoa – Kushirikiana – Kuomba - Kushuhudia - Kuhubiri - Kujifunza
6. Biblia - Sadaka
7. Furaha
8. Jina la kanisa la mtoto
9. Jina la mchungaji wa mtoto
10. Kutoa - Kuimba - Kujifunza
    kuliweka - wengine – kuhudhuria pamoja nawe

## Somo la 6

Ukurasa 29: Jina la Mtoto

1. Marko 5:19
2. Ndiyo - Hapana – Ndiyo – Ndiyo
3. X - Soma Biblia kila siku
   X - Waambie wengine kuhusu Yesu
   X - Ishi maisha ya Kikristo mbele ya wengine
4. Waalike kanisani na Wape trakti
5. Waweze kumjua Yesu na kuokolewa
6. Andika orodha ya watu 3 ambao utazungumza nao kuhusu Yesu
7. Jua ya kuwa Mungu anawapenda
   Jua ya kuwa sote tumetenda dhambi
   Jua ikiwa tukizikiri dhambi zetu Mungu ni mwaminifu atatusamehe
8. Mathayo 21:22
   Yohana 5:23
   Yohana 3:16
   Warumi 3:23
   1 Yohana 1:9
   Warumi 6:23
9. Pitia mistari uliyojifunza kwa moyo
10. Kukariri

# Kutumia Kikaragosi Katika Kufundisha Watoto

Vikaragosi ni njia bora inayoweza kutumiwa kufundisha kwa njia ya kuona. Inapotumiwa kwa usahihi, huchukua mawazo na shauku ya wale wanaosikiliza au kutazama. Kikaragosi kinaweza kutumika kwa matangazo, nyimbo, michezo, hadithi, kukariri, maelekezo, na kwa kujifurahisha tu.

KUMBUKA: Unapofundisha kuhusu wokovu, ni muhimu usiseme kwamba kikaragosi kimeokolewa au hakijaokolewa. Kikaragosi kinaweza kufundisha vitendo sahihi au ambavyo si sahihi / au tabia ya Kikristo. Lakini ukisema vina wokovu unaweza kuwachanganya watoto kwa sababu kikaragosi sicho halisi - lakini wokovu ni halisi.

## Kikaragosi ya Children's Gospel Box



Kwa sababu kikaragosi ya Children's Gospel Box hakiina mdomo unaoweza kusogeshwa, harakati kwa kikaragosi ndicho kitu ambacho kitawafurahisha watoto. Kuhamisha kikaragosi hicho polepole ndiyo inatengeneza mazingira kwamba kikaragosi kinazungumza.

### Hapa kuna mambo machache ya kufikiria:

- Kumbuka kuliangalia darasa mara kwa mara na hakikisha kikaragosi hicho nacho kinalitazama darasa.
- Fanya kikaragosi kisogee, kana kwamba kipo hai. Ikiwa mkono ndani ya kikaragosi umelegea, itaonekana kama kikaragosi kimekufa.
- Wakati kikaragosi "kinazungumza" hakikisha unakuwa makini.
- Kichwa kilicho kinamishwa kinaonyesha huzuni, na mwendo wa polepole kinaonyesha huzuni na / au usingizi. Kusonga kichwa upande kwa upande kinaweza kuashiria hali ya kutokubaliana. Kichwa, ikilala upande mmoja kinaonyesha wasiwasi au machafuko.

## Kikaragosi Kilicho Kimya

Vidokezo vingi hapo juu vinatumika kwa "Kikaragosi kilicho kimya." Kikaragosi hata hivyo kinaongea tu na kiongozi, na kiongozi analiambia darasa. Kwa mfano, kikaragosi kinaangalia darasa na kukimbilia kwa mwalimu na kuweka kichwa chake kwenye bega la mwalimu. Mwalimu anakiliza kwa kunong'ona, "Kuna nini?" Kikaragosi "kinamnong'oneza" mwalimu kuwa kina wasiwasi ikiwa kiko mbele ya watu hawa wote. Kisha mwalimu anaelezea kuwa hakuna kitu cha kuogopa.

## Kikaragosi Mwenye Mdomo Unaoweza Kusogea

- Unda sauti kwa ajili ya kikaragosi chako.
- Sawazisha ufunguzi wa mdomo wa kikaragosi na neno linalonenwa. Usifungue mdomo kabisa kwa njia ile ile kwa kila neno. Tumia mdomo unaofunguliwe sana wakati wa kuzidisha au wakati wa kuongea sauti kubwa. Kinywa cha kikaragosi kinaweza kubaki wazi kidogo wakati wa kusikiliza. Hii inaweza kuwakilisha "tabasamu."  Wakati unapofunga mdomo wa  kikaragosi kwa nguvu ikionyesha hasira.

**Kwa Kikaragosi CHOCHOTE: Mazoezi! Fanya mazoezi!**
**Fanya mazoezi... mbele ya kioo kama ikiwezekana!**

Hapa kuna chaguzi aina mbili za jinsi kikaragosi kinaweza kusimulia hadithi ya Biblia. Hizi ni sampuli ya mwalimu 1 na kikaragosi 1

### # 1: Hadithi ya Yona (Yona 1-3)

Kikaragosi: Hamjambo watoto! Je! Umewahi kwenda kuvua samaki? Ulikamata samaki wowote? Leo tutajifunza kuhusu samaki aliyemkamata mtu!

Siku moja, Mungu alizungumza na mtu mmoja anayeitwa Yona na kumwambia aende katika mji uitwao Ninawi kuhubiri ujumbe maalum. Mungu alitaka watu pale wajue kuwa alikuwa na hasira kwa sababu ya mambo mabaya ambayo wamekuwa wakifanya.

Lakini Yona hakutaka kwenda Ninawi. Alijaribu kumkimbia Mungu kwa kuingia kwenye meli. Meli ilienda, lakini Mungu alijua Yona alipokuwapo. Alituma dhoruba kubwa na kutikisa meli kiasi cha kutaka kuiharibu. Kila mtu kwenye meli aliogopa sana.

Yona aliwaambia wengine kwamba Mungu ndiye aliyetuma dhoruba ya kumzuia kukimbia. Wakamwuliza wafanyeje kuzuia dhoruba. Hawakutaka hasira ya Mungu kwao wote. Basi, Yona aliwaambia wamtupe kwenye maji.

Mwanzoni, wanaume hao hawakutaka kufanya hivyo kwa Yona. Waliweka jitihada zaidi ya kupiga makasia kuliko hapo awali ili kufika pwani, lakini hawakuweza kufika hapo. Dhoruba ilizidi kuwa mbaya. Mwishowe, waliomba Mungu awasamehe, na wakamtupa Yona ndani ya maji. Mara tu walipofanya hivyo, bahari ikatulia kabisa, na wanaume wote wakamwamini Mungu.

Wakati Yona alipofika ndani ya maji, samaki mkubwa, aliyetumwa na Mungu, akamjia na kummeza. Yona aliogopa na akasali kwa Mungu. Baada ya siku tatu ndani ya samaki, Mungu akamfanya samaki kumtapika Yona pwani!

Yona alifurahi sana kuwa nje ya tumbo la samaki. Alikwenda moja kwa moja Ninawi na kuwahubiria watu. Aliwaambia kuwa walikuwa na siku 40 za kubadilisha tabia zao na kufanya yaliyo mema, au Mungu angeharibu mji wao. Watu wote katika mji huo mkubwa walimwamini Mungu na kumwambia Mungu kwamba awahurumie. Kwa sababu Yona alihubiri na watu waliamini, mji wote uliokolewa!

Mwalimu: Kumbe! (ingiza jina la kikaragosi)! Hiyo ni hadithi nzuri na ya kweli kutoka kwenye Biblia! Nimefurahi kwamba mwishowe Yona alimtii Mungu. {Sasa mwalimu anafundisha inavyohusiana na leo...}

## # 2: Hadithi ya Danieli kwenye Tundu la Simba (Danieli 6)

Mwalimu: Habari watoto! Je! Umewahi kuwa na njaa kweli kweli? Njaa kama ya simba, labda? Nina hadithi kuhusu simba fulani ambao walikuwa na njaa sana, lakini hawakupata chakula cha jioni walichotaka. Na labda rafiki yangu (ingiza jina la kikaragosi hapa) angependa kusikia pia. Je! Ungependa kusikia hadithi hii ya kweli kutoka katika Biblia?

Kikaragosi: {Kinatikisa kichwa kuonyesha ndiyo}

Mwalimu: Katika Agano la Kale, tunapata hadithi ya nabii mkubwa aliyeitwa Danieli ambaye aliishi Babeli. Danieli alimpenda Mungu na alikuwa akimwomba mara kadhaa kwa siku. Mungu alikuwa amempa Danieli kazi ya pekee ya kumsaidia mfalme, jina lake Dario. Wanaume wengine walimwonea wivu Danieli kwa sababu walitaka kazi hiyo. Je! Hawa wanaonekana kama wanaume wazuri?

Kikaragosi: {Kinatikisa kichwa kuonyesha hapana}

Mwalimu: Hiyo ni kweli. Sio fadhili kabisa. Kwa kweli, wanaume wenye wivu walikwenda kwa mfalme na wakazungumza naye kwa kufanya sheria maalum. Sheria ilisema kwamba kwa siku 30, hakuna mtu anayeruhusiwa kuomba kwa miungu yoyote na kuwaomba vitu vyovyote. Ikiwa wanahitaji kitu, wangekuja kumwomba mfalme badala yake. Wanaume hao walisema kwamba sheria hii itasaidia watu kuona jinsi mfalme wao alivyo mkubwa na ni kiasi gani anaweza kuwasaidia watu wake. Ikiwa mtu angevunja sheria, wangelishwa kwenye kundi la simba wenye njaa. Mfalme Dario alijua kuwa Danieli alimpenda Mungu wake na alikuwa akisali kila siku, lakini hakufikiria juu ya hilo wakati akisaini sheria mpya.

Halafu siku moja, wanaume wenye wivu walimshika Danieli akiomba Mungu na wakakimbilia moja kwa moja kwa Mfalme Dario ili wamwambie. Je! Unafikiria Mfalme Dario alijisikiaje?

Kikaragosi: {kinamisha kichwa chini ili kuashiria huzuni}

Mwalimu: Ndiyo, alijisikia huzuni. Mfalme Dario alimpenda Danieli na hakutaka kumrusha kwenye simba. Alijaribu siku nzima kutafuta njia ya kumwokoa Danieli, lakini kwa kuwa sheria iliwekwa, ilibidi kutii. Kwa kusikitisha, mfalme aliwaambia walinzi wake wamtupe Daniel ndani ya pango lililojaa simba wenye njaa. Mfalme Dario akamwambia Danieli, "Najua ya kuwa Mungu wako atakuokoa." Kisha jiwe kubwa likatikiswa juu ya mlango wa shimo. Je! Unafikiria Daniel angehisije?

Kikaragosi: {Kinatikisa upande upande kuonyesha wasiwasi}

Mwalimu: Kweli usiku huo, mfalme alikuwa na huzuni sana. Hakula, hakusikiza muziki, na hakuweza hata kulala. Alichoweza kufanya ni kufikiria kuhusu rafiki yake, Danieli. Mara tu asubuhi yenye mwanga, Dario alikimbilia pangoni. "Danieli, Je! Mungu wako amekuokoa?" aliuliza.

Danieli alijibu kwa furaha. "Mungu wangu alimtuma malaika kufunga midomo ya simba wenye njaa." Alimwambia Mfalme Dario hana hatia na hataweza kufanya chochote kumwumiza mfalme. Mfalme Dario alijua hii ni kweli. Alikuwa na furaha sana kwa Danieli. Basi mfalme akamwachilia huru Danieli! Kisha akaamuru watu ambao walikuwa wamemdanganya watupwe kwenye simba. Mfalme Dario alitangaza sheria mpya kwenye ufalme wote kwamba kila mtu anapaswa kumwabudu Mungu aliye hai. Je! Unafikiria Danieli na mfalme walijisikiaje sasa?

Kikaragosi: {Kinaruka juu na chini kuonyesha msisimko}

Mwalimu: Hiyo ni kweli! Mungu alikuwa mwaminifu kumwokoa Daniel, na walifurahia sana! {Sasa mwalimu anafundisha inavyohusiana na leo...}

# Kitabu cha Injili Isiyo na Maneno na Bangili

**DHAHABU** Rangi ya dhahabu inatukumbusha Mbingu. Biblia inatuambia kuwa Mbingu ina barabara ya dhahabu! Lakini jambo nzuri kuhusu Mbingu ni kwamba Mungu, aliyekuumba wewe na mimi, anaishi hapo. Biblia, Neno la Mungu, linasema, "Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee lakini awe na uzima wa milele" (Yohana 3:16). Yesu, Mwana wa Mungu, yuko Mbinguni akitayarisha mahali kwa wote wamwaminio (Yohana 14:23). Mungu ni mtakatifu na mkamilifu. Hawezi kuruhusu kitu chochote mbinguni ambacho si kikamilifu, kwa hivyo kuna kitu kimoja ambacho hakiwezi kuwa Mbinguni. Je! Unaweza kufikiria kinaweza kuwa nini?

**NYEUSI** Ni dhambi. Hiyo ndio rangi ya giza inachotukumbusha. Dhambi ni kitu chochote tunachofanya kisichompendeza Mungu, kama kusema uwongo, kudanganya, kuwa mbinafsi, kutotii, au kuumiza wengine. Biblia inasema, "kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Warumi 3:23). Hiyo inamaanisha kila mtu - mkubwa au mdogo, mchanga au mzee! Haijalishi unaishi wapi au wewe ni nani, umefanya dhambi. Kila mtu amezaliwa na "hamu ya" kufanya vibaya. Mungu anasema kwamba dhambi lazima iadhibiwe (Warumi 6:23) na adhabu ya dhambi itenganishwe na Mungu milele mahali pa mateso, mahali paitwapo Kuzimu. Lakini, Mungu ana mpango mzuri sana ili usilazimike kuadhibiwa kwa dhambi zako!

**NYEKUNDU** Mungu alimtuma Yesu Kristo, Mwana Wake mkamilifu, kuzaliwa kama mtoto mdogo. Yesu aliishi maisha makamilifu; Hakuwahi kufanya dhambi. Alipokuwa mtu mzima, watu waovu walimpachika msalabani. Rangi hii nyekundu inatukumbusha damu ya Yesu ambayo alipoteza msalabani. Biblia inasema kuwa bila kutoa damu, hakuna msamaha wa dhambi (Waebrania 9:22). Kwa hivyo, Yesu Kristo alikufa kwa hiari kuchukua adhabu ya dhambi yako. Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, akazikwa, na kisha akainuka tena siku ya tatu, kama vile Biblia inavyosema (1 Wakorintho 15:34). Sasa, kwa sababu ya alichotufanyia Yesu, unaweza kusamehewa dhambi zako.

**NYEUPE** **ni kama giza la dhambi mioyoni mwetu huoshwa kabisa, kama rangi hii. "Dhambi zetu zimeoshwa, na tumesafishwa kwa sababu Kristo alitoa mwili wake mwenyewe..." (Waebrania 10:10). Kwa hivyo unawezaje kuwa na moyo safi?**

K = Kiri: Kiri kwa Mungu wewe ni mwenye dhambi na unataka kuachana na dhambi hizo. “Ikiwa tunakiri dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki kutusamehe dhambi zetu na kutusafisha dhidi ya udhalimu wote" (1 Yohana 1:9).

A = Amini: Mwamini Yesu Kristo, ya kuwa ni Mwana mkamilifu wa Mungu ambaye alikufa kwa ajili ya dhambi zako, akazikwa, na akarudi hai.

C = Chagua: Mchague Yesu kuwa Bwana wa maisha yako!

Je! Ungependa kufanya hivyo sasa hivi? Mungu ameahidi kusikia, na kukuleta katika familia Yake. Chukua muda kidogo na uzungumze na Mungu sasa hivi. Itabadilisha maisha yako milele!

**KIJANI** Rangi ya mwisho inawakilisha vitu ambavyo hukua. Unapomwomba Mungu akusamehe na kukuokoa, unakuwa mtoto wake. Mara tu ukiwa mtoto wake, hatakuacha kamwe (Waebrania 13:5). Na Mungu anataka watoto wake wamjue yeye bora na kukua na kuwa kama Yeye.

Vitu hivi vinne vitakusaidia kukua:

1. Omba (zungumza na Mungu kila siku).
2. Soma na uitii Biblia (kujua anachosema kisha ufanye).
3. Waambie wengine kuhusu Yesu.
4. Nenda kwenye kanisa la wanaoamini Biblia (ambapo unaweza kujifunza zaidi juu yake).

**Mwombe Mungu akusaidie kuishi maisha yanayompendeza! Shiriki habari njema za rangi hizi na mtu mwengine!**

# Vijiti vya Sifa

Kijiti kinajumuisha kibomba cha plastiki na vipande vinne vya inchi 12 vya riboni za rangi tofauti tofauti. Shikiza riboni kwenye kilele cha kibomba. Ikiwa vishikizo havipatikani, funga vipande vya riboni pamoja, na kisha funga seti juu ya kibomba au kifimbo salama.

Chagua kikundi cha watoto kisimame mbele ya watoto wengine ili kusaidia kuongoza wakati wa sifa. Wape watoto waliopo mbele vijiti vya sifa na ikiwa kuna vijiti vya kutosha, watoto waliobaki wanaweza kupokea kimoja kimoja pia.

Ni muhimu kufanya kazi na kikundi cha watoto ambao wamechaguliwa kuongoza, kwa kuwahimiza kupeperusha vijiti kwa kufuata namna ya wimbo na kila mtu kwa mwenzake.

Tumia fursa hii kufundisha watoto jinsi ya kutumia vinywa vyao kusifu, wakisema maneno kama, "Asifiwe Bwana!" au "Tunakusifu, Ee Mungu!"



# Tic Tac Toe


## Jinsi ya Kutengeneza Mchezo

### Vitu vinavyohitajika kutengeneza ubao wa mchezo:

- Mraba mmoja wa vitambaa maalumu (inchi 9 x 9 au 12 x 12)
- inchi 1.5 katika kipenyo cha kitambaa maalumu cha mraba chenye rangi mbili tofauti (mraba 5 ya kila rangi)
- Kalamu ya kudumu au mkanda ya umeme (kuunda mistari ya kugawa)

### Maagizo ya kutengeneza ubao wa mchezo:

1. Tumia kalamu au mkanda wa umeme, chora mistari miwili ya wima kwenye kitambaa maalumu cha mraba. Hii itakuwa imegawanya mraba katika sehemu tatu.
2. Halafu, tengeneza mistari mingine miwili, iliyowekwa sawa, ikienda sambamba kwenye kitambaa maalumu. Hii itakuwa imegawanya mraba katika sehemu tisa.



# Jinsi ya Kucheza Mchezo

Wagawanye watoto katika timu mbili. Wape kila timu seti ya mraba ya rangi moja. Watacheza dhidi ya kila mmoja. Majibu sahihi huruhusu timu kuweka moja ya viwanja vyao kwenye ubao wa mchezo. Kama ilivyo kawaida ya Tic Tac Toe, yule anayepata vipande vitatu (3) mfululizo hushinda (3 ya kwenda upande kwa upande, 3 ya kwenda chini, au 3 kwenda kona kwa kona). Timu inayopingana inapaswa kujaribu kuzuia 3 mfululizo wa mpinzani wao. Hii ni njia ya kufurahiya na watoto!

Mchezo unaweza kutumika kwa njia kadhaa. Hapa kuna chaguzi chache:

**Kama marudio ya somo**

Timu moja huulizwa swali linalohusiana na somo lililofundishwa. Ikiwa mtu kwenye timu hiyo anajibu swali kwa usahihi, huweka mraba wa rangi kwenye ubao. Timu nyingine inapata swali linalofuata, na kucheza huendelea hadi timu moja itapata 3 mfululizo.

**Kama marudio ya mstari wa kukariri**

Timu moja huanza na inajaribu kusema mstari kikamilifu ili kuweka mraba kwenye ubao. Halafu huenda na kurudi timu kwa timu, na watoto wengi wakirudia mstari hiyo. Vinginevyo, watoto wanaweza kuwajibika kwa kusema tu neno LINALOFUATA tu kwenye mstari kwa usahihi, badala ya kurudia kifungu chote.

# Karatasi ya Mipango ya Somo

▷ Anza Jumatatu kwa mafundisho yako ya Jumapili.

▷ Mwombe Mungu akuongoze katika kuliandaa somo lako.

▷ Amua Andiko gani au Hadithi ya Biblia itakayojifunzwa.

## #1 Andiko au Hadithi ya Biblia:

▷ Soma maandishi mara mbili.

▷ Soma maandishi kwa mara ya tatu, ukiandika matukio ya mstari wa hadithi. Hizi ni vitendo vinavyotakiwa kwenye hadithi au sehemu muhimu ya kufundishwa.

## #2 Matukio ya Hadithi

1. 
2. 
3. 
4. 
5. 
6. 
7. 

## #3 Misaada ya kuona ya Biblia iliyo ubunifu:

(Jinsi ya kuelezea hadithi ya Biblia kwa ubunifu, kwa mfano: flannel graph, kikaragosi, sanaa, ishara za mikono, viwasilishi, nk.)

## #4 Mstari wa Kukariri:

## #5 Mchezo wa Mstari wa Kukariri:

## #6 Je! Mtoto ambaye hajaokoka anapaswa kufanya nini na somo hili?

## #7 Je! Mtoto aliyeokoka anatakiwa kufanya nini na somo hili?

## #8 Je! Ni jambo au mfano gani wa kufundishia au kuimarishia hiyo hatua ya kivitendo?

## #9 Maswali ya Marudio

1. ______________________________

2. ______________________________

3. ______________________________

4. ______________________________

5. ______________________________

6. ______________________________

7. ______________________________

8. ______________________________

9. ______________________________

10. ______________________________

## #10 Mazoezi & Maombi!

- ▷ Fanya mazoezi ya kufundisha somo kwa sauti angalau mara mbili kwa KUTUMIA misaada ya kuona. Fanya hadithi iwe hai, badilisha sauti yako, tumia kiboresha sauti, nk. Usisome tu somo kwenye karatasi yako!
- ▷ Kuwa na ustadi wa kusimulia. Tengeneza swali au taarifa ambayo itavutia shauku ya mtoto tangu mwanzo.
- ▷ Muhimu zaidi, WAOMBEE WATOTO! Mwombe Roho Mtakatifu akuongoze unapoitafakari kuhusu maandishi na unapozungumza Neno la Mungu. Ombea miyoyo ya watoto iwe wazi kwa ajili ya matumizi ya Maandiko.











CHILDREN'S gospel box

©2018

Children's Gospel Box Training Resources—Swahili